Jarida la

# Pika kwa Umeme

**Toleo namba 01** | Septemba **25, 2025**






**PIKA KWA UMEME** – Jarida hili linaelimisha juu ya matumizi sahihi ya Nishati safi ya kupikia kwa umeme, ikiwa ni njia salama na gharama nafuu .

Lengo kuu ni kuwahamasisha Watanzania kuchagua umeme kama nishati bora na rafiki wa mazingira, huku tukihakikisha afya, ufanisi na ustawi wa jamii

Pata Taarifa mbalimbali za **TANESCO** kupitia Whatsap Channel TANESCO YETU kwa Kuscan **QR CODE**

# BODI YA WAHARIRI


| | | |
|---|---|---|
| 01. | **Lazaro J. Twange** | - Mwenyekiti |
| 02. | **Irene Gowelle** | - Mhariri Mkuu |
| 03. | **Augustino Kasale** | - Mhariri |
| 04. | **Robert Fredy** | - Mwandishi |
| 05. | **Joyce William** | - Mwandishi |
| 06. | **Happiness Njovu** | - Mwandishi |
| 07. | **Donasian John** | - Mwandishi |
| 08. | **Angeline Bidya** | - Mwandishi |
| 09. | **Goodluck Assenga** | - Mwandishi |
| 10. | **Esta Msaki** | - Mwandishi |
| 11. | **Josephine Mtamakaya** | - Mwandishi |
| 12. | **Kelvin Kasambala** | - Mwandishi |
| 13. | **Christina Shoki** | - Mwandishi |
| 14. | **Michael Sokotta** | - Msanifu Kurasa |




# YALIYOMO NDANI YA **JARIDA**










**Uk 6.** ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YATOLEWA KWA WAFANYAKAZI WA TANESCO MKOA WA MARA

**Uk 7.** TANESCO MTWARA WAENDELEA NA ELIMU YA NISHATI SAFI KWA WAFANYAKAZI

**Uk 8.** WILAYA ZA MAFINGA NA KILOLO ZANUFAIKA NA ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KWA UMEME

**Uk 9.** TANESCO RUKWA YATOA ELIMU YA NISHATI SAFI KWA WAFANYAKAZI WAKE WA WILAYA YA SUMBAWANGA MJINI

**Uk 10.** WAJASIRIAMALI TEMEKE WAHAMASIKA NA MATUMIZI YA MAJIKO YA NISHATI SAFI YA UMEME

**Uk 13.** TANESCO MKOA WA PWANI KUSINI YAHAMASISHA MATUMIZI YA NISHATI SAFI KWA KUGAWA MAJIKO KWA VIONGOZI WA WILAYA YA KIBITI

**Uk 15.** WAFANYAKAZI WAFURAHIA ELIMU KUHUSU NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Uk 16.** MAJIKO JANJA YA KUPIKIA KWA UMEME YAWAFIKIA WAFANYAKAZI MOROGORO

**Uk 17.** KYELA YAVUTIWA NA MAJIKO JANJA YA UMEME KAMA NISHATI SAFI JIKONI

**Uk 18.** NISHATI SAFI, YAIFIKIA SONGWE

**Uk 20.** NACHINGWEA , LIWALE NA KILWA WAFUNGUA UKURASA MPYA KATIKA NISHATI YA KUPIKIA





Pressure Cooker



Air Flyer



Rice Cooker

# UMEME NISHATI NAFUU ZAIDI JIKONI

- Huokoa muda jikoni
- Ni salama kwa matumizi
- Hulinda afya, haitoi moshi
- Hutunza mazingira
- Ni safi jikoni
- Ni gharama nafuu mno



# ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YATOLEWA KWA WAFANYAKAZI WA TANESCO MKOA WA MARA

Na Joyce William, Mara

Wafanyakazi wa Shirika la Umeme (TANESCO) Wilaya ya Musoma mkoani Mara wamepata elimu ya Nishati safi ya kupikia kwa vitendo kutoka kwa Afisa Uhusiano na Huduma kwa wateja Bi. Joyce William leo tarehe 29 Agosti, 2025 katika Ofisi za Mkoa TANESCO Mara.

Wafanyakazi hao wameweza kuelezewa umuhimu wa Nishati safi ya kupikia kwa umeme na faida zake.

Vilevile, Afisa Rasilimali watu wa Mkoa Ndg. Duncan Faraja Mwankupili alizungumza na wafanyakazi kuhusu mkakati wa Shirika wa kuhakikisha wafanyakazi wote wanapata majiko ya kupikia kwa mkopo kwa njia ya Ruzuku ili kuwawezesha kuwa mfano bora na mabalozi kwa watu wengine.

Sambamba na hilo utaratibu umetolewa kwa wafanyakazi wa namna ya kupata majiko hayo na wengi kuonekana kufurahishwa na mpango huo wa Shirika wa kulipia kwa mkopo na kuongeza shauku ya uhitaji.

Aidha, wafanyakazi wameomba upatikanaji wa haraka wa majiko mengine ili kukidhi mahitaji yaliyopo.





# TANESCO MTWARA WAENDELEA NA ELIMU YA NISHATI SAFI KWA WAFANYAKAZI

**Na Happiness Njovu,** Mtwara

Katika kuendelea na jitihada za kuhakikisha kila mfanyakazi wa TANESCO anakuwa Balozi wa Nishati Safi ya Kupikia Ofisi ya Uhusiano na Huduma kwa wateja pamoja na Ofisi ya Rasilimali watu Mkoa wa Mtwara ziliandaa mafunzo maalumu kwa wafanyakazi kuhusu matumizi ya Nishati Safi ya kupikia ya umeme pamoja na faida zake.

Elimu hiyo ilitolewa siku ya Alhamisi ya tarehe 28 Agosti 2025 na kuhusisha wafanyakazi wote wa Ofisi ya TANESCO Mtwara.

Wafanyakazi wa Mkoa wa Mtwara wameifurahia elimu hiyo na kuahidi kuwa mabalozi wazuri wa matumizi na nishati safi ya kupikia kwa umeme na kuomba uongozi kuharakisha awamu ya pili ya ugawaji wa majiko hayo kwani uhitaji ni mkubwa kuliko majiko yaliyotolewa.





# WILAYA ZA MAFINGA NA KILOLO ZANUFAIKA NA ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KWA UMEME

**Na Donasian John,** Iringa

Shirika la Umeme Tanzania, (TANESCO) Mkoa wa Iringa limetoa elimu juu ya matumizi ya umeme katika wilaya za TANESCO za Kilolo na Mafinga Mkoani Iringa.

Elimu hiyo imetolewa Agosti 28, 2025, na Maafisa uhusiano na huduma kwa wateja wa Mkoa wa Iringa kwa lengo la kuwaelimisha wananchi juu ya huduma za TANESCO na matumizi ya Nishati safi ya kupikia ya Umeme ikiwa ni muendelezo wa Kampeni ya Kitaifa ya kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia.

Akizungumza na wananchi hao Maafisa Uhusiano na huduma kwa wateja wa wilaya ya Kilolo na Mafinga Bw. Joseph Sungura na Philemon Kaseka wamewaelemisha wananchi hao kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme pamoja na kuzingatia usalama wao wanapotumia umeme na usalama wa miundombinu ya umeme.

Akiwaasa kuhusu mwenendo wao wa kikazi, aliwakumbusha kuwa TANESCO imepiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma bora kwa wateja, hivyo wanapaswa kuendeleza juhudi hizo kwa kuwahudumia wateja kwa kuwajibika na kuwa na maadili ya hali ya juu.







# TANESCO RUKWA YATOA ELIMU YA NISHATI SAFI KWA WAFANYAKAZI WAKE WA WILAYA YA SUMBAWANGA MJINI

Na **Angeline Bidya,** Rukwa

TANESCO Mkoa wa Rukwa imeendesha mafunzo ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme kwa wafanyakazi 58 tarehe Agosti 29, 2025. Mafunzo hayo ambayo yalifunguliwa na Meneja wa Mkoa Mha. Johnson Mwigune, yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mkoa na kutolewa na Afisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, Afisa Rasilimali Watu pamoja na Mhasibu wa Mkoa.

Katika mafunzo hayo, wafanyakazi walipata elimu ya vitendo juu ya matumizi ya majiko sanifu ya kupikia ya umeme na kupatiwa utaratibu wa kuyanunua kwa bei ya ruzuku ambapo jumla ya wafanyakazi 13 walifanikiwa kuyalipia majiko hayo, (7 kwa fedha taslimu na 6 kupatiwa namba za malipo) huku zaidi ya watumishi 25 wakionyesha nia ya kuyahitaji kwa uharaka.

Wafanyakazi walieleza furaha yao baada ya kupata elimu hiyo na kuahidi kuwa mabalozi wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme kwa jamaii na kutoa elimu ya faida zake kwa afya, uchumi na mazingira.





# WAJASIRIAMALI TEMEKE WAHAMASIKA NA MATUMIZI YA MAJIKO YA NISHATI SAFI YA UMEME

Na **Goodluck Assenga,** Temeke

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Temeke limeshiriki Kongamano la Nishati Safi lililoandaliwa na Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania kwa kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wajasiriamali wadogo zaidi ya 70 wakiwemo Mama Lishe, Baba Lishe na makundi mengine ya wafanyabiashara wadogo ambapo kati yao 20 wamejiorodhesha kupata majiko hayo.

Akizungumza wakati wa kongamano hilo lililofanyika Agosti 30, 2025 katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Kibasila, Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, Afisa Huduma kwa Wateja, Bw. Goodluck Assenga ameeleza kwamba Umeme ni nishati nafuu zaidi jikoni.

"Kwa kutumia vifaa sahihi vya umeme, nishati hii inaokoa muda jikoni, inatunza mazingira na ni rafiki kwa mtumiaji kwa kuwa ni salama," alifafanua zaidi Bw. Goodluck

Aidha, wajasiriamali hao walijifunza kwa vitendo namna majiko hayo yanavyofanya kazi kwa kupika vyakula mbalimbali kwa urahisi na haraka.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN) Mhe. Janeth Mbene, ambaye aliipongeza TANESCO mkoa wa Temeke kwa juhudi za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme.



# MATUKIO KATIKA PICHA

ELIMU YA NISHATI SAFI YAFIKA KWENYE KONGAMANO LA WAJANE LA KUWAINUA KIUCHUMI





JIUNGE NA TANESCO HUDUMA

# WHATSAPP



## Je, unajua?

Kupitia magroup haya unaweza:👇🏽

- Kutoa taarifa kwa haraka
- Kupokea taarifa
- Kupata elimu na huduma bora bila kupiga simu au kufika ofisini

Huduma bora. Taarifa kwa wakati
Elimu kwa Urahisi



# TANESCO MKOA WA PWANI KUSINI YAHAMASISHA MATUMIZI YA NISHATI SAFI KWA KUGAWA MAJIKO KWA VIONGOZI WA WILAYA YA KIBITI

**Na Esta Msaki -** Pwani Kusini

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ) Mkoa wa Pwani Kusini ukiongozwa na Mha. Anita Marco ,Septemba15,2025 wametoa elimu ya Nishati safi ya kupikia ya Umeme kwa viongozi wa Serikali za mitaa, Wilaya ya Kibiti.

Katika elimu hiyo TANESCO imetoa majiko janja na yanayotumia umeme kidogo kwa Mkuu wa wailaya Kibiti, kama balozi wa kuhamasisha wa kuhamasisha wana Kibiti kutumia Nishati safi ya kupikia ya Umeme sawa sawa na Sera ya Serikali ya kuwataka wananchi kutumia nishati safi ya kupikia na kuachana na Nishati ambazo sio safi.

Akizungumza na Watendaji hao wa Wilaya ya Kibiti Mhandisi Anita Marco amesema kuwa TANESCO inaungana na Serikali katika kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya Nishati safi ya kupikia, hasa Umeme kama nishati Safi,Salama na Sanifu.

“Tunatekeleza malengo ya serikali ya kuhakikisha kila Mtanzania anatumia nishati safi hivyo tumewaletea viongozi wa wilaya kupitia uongozi.wenu mtatusaidia kuhamasisha watumishi wa chini kuweza kutumia nishati safi ya kupikia kwakuwa umeme ndio Nishati nafuu zaidi jikoni” alisema Mha. Anita

Akizungumza baada y kukabidhiwa jiko, Mkuu wa Wilaya ya Kibiti Mheshimiwa Kanali Joseph Kolombo ameishukuru TANESCOa kwa jitihata wanazozifanya za Uhamasishaji,na kuahidi kuzingatia kuwa wilaya yake itakua ya kuigwa Kwa matumizi mazuri ya Nishati Safi ya kupikia , kauli iliyoungwa mkono pia na Katibu Tawala wake Bi Maria Katemana ambaye amesema kuwa kwa pamoja watakua mabalozi wazuri wa nishati safi kwa kutumia majiko ya Umeme kama Nishati bora kwa kupikia.




TANESCO
180
Mchongo ni
Piga bure tukuhudumie
Namba yetu mpya ya huduma
kwa **wateja** bila malipo.
www.tanesco.co.tz



# WAFANYAKAZI WAFURAHIA ELIMU KUHUSU NISHATI SAFI YA KUPIKIA

**Na Josephine Mtamakaya -** Kinondoni Kusini

Katika Jitihada za kuhamasisha matumizi ya Nishati Salama na rafiki wa Mazingira, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Kinondoni Kusini Wilaya ya Magomeni limeendesha mafunzo ya Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia kwa Wafanyakazi.

Afisa Huduma kwa Wateja, Bi. Josephine Mtamakaya, Pamoja na Timu yake walitoa elimu hiyo Septemba 17,2025 kwa njia ya Vitendo, wakionyesha jinsi Majiko Janja yanavyoweza kupika kwa Haraka, kwa Gharama nafuu na kwa Usalama zaidi ikilinganishwa na Nishati Nyingine.

Bi. Mtamakaya aliwahimiza Wafanyakazi kuwa Mabalozi wazuri kwa kutumia Nishati Safi na Salama ili kulinda Mazingira, Kuokoa muda na kuhakikisha Afya bora kwa Watumiaji.

Wafanyakazi walionesha kufurahishwa na elimu waliyopewa na wengi wao waliahidi kununua na kutumia Majiko hayo, ili wawe mfano bora kwa Jamii katika kuhamasisha Matumizi ya Nishati Safi na Salama. na kupunguza Matumizi ya nishati zinazohatarisha Afya na Mazingira, na badala yake kuchagua suluhisho za kisasa na rafiki wa Mazingira.






# MAJIKO JANJA YA KUPIKIA KWA UMEME YAWAFIKIA WAFANYAKAZI MOROGORO

**Na Kelvin Kasambala -** Morogoro Kaskazini

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Morogoro Kaskazini, imeendelea na Jitihada za kutoa elimu ya Matumizi ya Nishati safi ya kupikia ya umeme kwa wafanyakazi wa Mkoa huo.

Akizungumza na wafanyakazi Septemba 15,2025 Meneja wa TANESCO Mkoa wa Morogoro Kaskazini, Mhandisi Zawadi Athanus, amesema kama Wafanyakazi wa Shirika linalohusika na uzalishaji Umeme,Usafirishaji na Usambazaji Umeme wanao wajibu wa kuunga mkono jitihada za Serikali na Shirika katika kuhakikisha wanatumia Nishati ya umeme kupikia .

Aidha Mha.Zawadi amewakabidhi wafanyakazi majiko janja kama sehemu ya mpango wa shirika wa kusambaza teknolojia rafiki kwa mazingira na kupunguza gharama za matumizi ya nishati.

Zoezi hilo la ugawaji wa majiko limefanyika baada ya wafanyakazi hao kuonesha nia kwa kujaza fomu maalum ya maombi ya majiko na Katika awamu ya kwanza, jumla ya majiko janja 30 yamepokelewa na kugawiwa kwa waliokamilisha taratibu mapema.




Wafanyakazi waliopokea majiko wameeleza kufurahia mpango huo kwa kuwa utawasaidia kupunguza gharama za matumizi ya nishati zingine ambazo ni ghali kupikia na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wateja na wananchi wote

Mhandisi Athanus amesema ugawaji huo ni mwanzo tu na kwamba awamu zinazofuata zitawalenga wafanyakazi wengine wengi zaidi, huku akibainisha kuwa mpango huo utafika hadi wilayani kwa uratibu wa ofisi yake.

Ameongeza kwa kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji Lazaro Twange kwa kufanikisha upatikanaji wa majiko hayo kwa wafanyakazi, huku akisisitiza kuwa ni hatua kubwa katika kuunga mkono jitihada za kitaifa za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia umeme.



# KYELA YAVUTIWA NA MAJIKO JANJA YA UMEME KAMA NISHATI SAFI JIKONI

**Na Christina Shoki** – Mbeya

Shirika la Umeme Tanzania TANESCO imetoa elimu ya matumizi ya Nishati Safi ya kupikia ya Umeme kwa wananchi wa Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya.

Akizungumza wakati akitoa elimu kwa wananchi wa wilaya ya Kyela,Afisa Uhusiano na huduma kwa wateja Bi.Christina Shoki, amewataka wateja na wananchi kutumia nishati ya Umeme kupikia kama nishati salama na sanifu jikoni, elimu ambayo imepolewa kwa mwitikio mkubwa kwa wateja zaidi ya 50 kuonesha hamasa ya kununua majiko janja ya umeme ili waweze kutumia kama Nishati nafuu zaidi.

Aidha Kitengo cha uhusiano na huduma kwa wateja pia kilitoa elimu juu ya Utunzaji wa miundo mbinu ya Umeme,na kuhamasisha wananchi waweze kutunza miundombinu ya Umeme,ili kuwa na umeme wa uhakika kwani vitendo vya wizi na uharibifu wa miundombinu ya umeme unarudisha nyuma maendeleo ya Shirika na Serikali kwa ujumla.

Sambamba na hilo wananchi pia walipata elimu ya namna ya kupata huduma za TANESCo ikiwemo matumizi wa namba 180 na mfumo wa Nikonect.





# NISHATI SAFI, YAIFIKIA SONGWE

**Na Christina Shoki** – Mbeya

Wafanyakazi wa TANESCO Mkoa wa Songwe wamepata Elimu ya Matumizi ya Nisahati Safi ya Kupikia ya Umeme, ikiwa ni moja ya Ajenda ya Kitaifa ya kuondokana na Matumizi ya Nishati zingine na kutumia nishati safi ya kupikia.

Akizungumza wakati wa Mafunzo hayo Agost 28,2025 katika ukumbi wa Mikutano ofisi ya Mkoa Tanesco, Afisa Uhusiano na Huduma kwa wateja Bi Elfrida Nsulau amesema kuwa mafunzo hayo yamekusudia kuwapa elimu wafanyakazi juu ya matumizi ya Nishati safi ya Umeme, namna ilivyo rahisi na gharama nafuu, ili pia waweze kuwa mabalozi wazuri na kufikisha elimu hiyo kwa jamii,

Naye Afisa Rasilimali watu Bi Neema kombo Amesema kuwa katika kuhakikisha mpango mkakati wa matumizi ya Nishati safi ya kupikia yanaanza kwa wafanyakazi, Shirika limeandaa mpango wa kuwawezesha wafanyakazi kupata majiko ya Umeme kwa bei ya ruzuku

Katika mafunzo hayo wafanyakazi 25 wameweza kuchukua majiko ya Pressure cooker na wengine 38 pia wamehamasika kuchukua majiko janja bila mkopo

Jitihada za kuhamasisha matumizi ya Nishati safi kwa wafanyakazi, bado zinaendelea katika mkoa wa Songwe, lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wote wa Songwe wanapata elimu hii.



# MATUKIO KATIKA PICHA

ELIMU YA NISHATI SAFI YAFIKA **SONGWE**








# NACHINGWEA , LIWALE NA KILWA WAFUNGUA UKURASA MPYA KATIKA NISHATI YA KUPIKIA

**Na Robert Fredy -** Lindi

Katika kuunga mkono jitihada za mhe. Raisi wa Jamuhuri wa muungano wa Tanzania Dkt. Samia S. Hassan yakutokomeza nishati isiyo salama na safi ya kupikia idara ya uhusiano na huduma kwa wateja imeendesha zoezi la  ungawaji wa majiko ya ruzuku kwa wafanyakazi katika wilaya ya Nachingwea,Liwale pamoja na Kilwa.

Zoezi hilo limefanyika kwa tarehe 10 na 11 ya mwezi wa tisa 2025 ikihusisha mafunzo kwa njia ya vitendo kwa namna majiko hayo yanavyofanyakazi na faida zake zilizobainishwa na afisa huduma kwa Wateja Bw. Robert Fredy.

Wafanyakazi walioudhuria mafunzo hayo ni takribani 124, huku wafanyakazi waliweza kununua majiko hayo kwa njia ya mkataba ikiwa ni kumi na tatu (13) na fedha taslimu ni wawili (2) kwa wilaya zote tatu.

Hata hivyo, mwitikio kwa wafanyakazi wenye uhitaji wa majiko hayo baada ya mafunzo kuwa kubwa kwani waliohitaji walikuwa 47 kati ya wafanyakazi waliouhudhuria katika mafunzo hayo.

Aidha, wafanyakazi wote walitoa shukrani zao za dhati kwa Mkurugenzi mtendaji Bw. Lazaro Twange kwa kupata majiko yaliyo na ufanisi mkubwa katika maandalizi ya vyakulala mbalimbali na kutoa ahadi yakuwa mabolizi kwa wateja pamoja na umma kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Zoezi hili la ugawaji wa majiko kwa njia ya ruzuku liloanza tarehe 8/9/2025 limehitimishwa rasmi leo tarehe 11/9/2025 katika wilaya tano (5) kwa kugawa majiko ishirini na nane (28) katika wilaya ya Lindi (8) Ruangwa (5),Nachingwea (5),Liwale (5), na Kilwa (5).



# MATUKIO KATIKA PICHA

**NACHINGWEA , LIWALE** NA **KILWA** WAFUNGUA UKURASA MPYA KATIKA NISHATI YA KUPIKIA








# Umeme **Nishati** Nafuu Zaidi **Jikoni,** Pika kwa **Umeme**

Ni Gharama Nafuu

Itakufupishia Muda Jikoni

Ni Salama kwa Afya na Mazingira




Pika kwa Umeme

Pata **Taarifa** na **Huduma** Mbalimbali Kupitia **Mitandao** Yetu ya **Kijamii**




@tanesco_official_page

@tanescoyetu

@tanescoyetutz

www.tanesco.co.tz

0758 346 869



Limetolewa na:
Kurugenzi ya Mawasiliano na Huduma kwa Wateja,
**TANESCO** Makao Makuu, Dodoma.

**TANESCO YETU**
WhatsApp Channel

## FOLLOW US

www.tanesco.co.tz